## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOMBERO

**(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri)**

HALMASHAURI YA WILAYA KILOMBERO

Simu Na. 023 – 2625313
Fax Na. 023 – 2625046
Fax Na. 023 – 2625058
**Email-kilomberodc@yahoo.com**

Ofisi ya Mkur,ugenzi
S.L.P. 263,
**IFAKARA.**

**Unapojibu tafadhali taja;-**

Kumb.Na.**KB/LD. No. 161/19/SGM**

07/05/2018

Tafadhali husika na kichwa cha hapo juu pamoja na barua toka ofisi yako ya tarehe 28/12/2017 yenye Kumb Na. LD/CZ/7264/7.

Kwa barua hii tuwasilisha Memorandum na Articles of association ya Kampuni ya GRL TANZANIA LIMITED pamoja na rasimu za hati zilizo andaliwa kwa jina jipya la Kampuni la GRL TANZANIA LIMITED kwa hatua zaidi za usajili.

**Syabumi Godwin Mwaipopo**
Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero

**Nakala**
Green Resources Limited,
S.L.P 108
**MAFINGA**-Kwa taarifa

MAENDELEO YA MAKAZI
**IMEPOKELEWA**
13 SEP 2018
OFISI YA KAMISHNA MSAIDIZI
YA ARDHI - KANDA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOMBERO**
***(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)***

Simu: 023 - 2931523
Fax: 023 - 2931513
E-mail : ded@kilomberodc.go.tz
E-mail : psded@kilomberodc.go.tz

Idara ya Ardhi na Maliasili
S.L.P. 263,
**IFAKARA.**

**Unapojibu tafadhali taja:-**

Kumb Na. KDC/LD/87127/19/S.G.M

12/09/2018

Kamishna Msaidizi wa Ardhi,
Kanda ya Kati
S.L.P 1062,
**40477 DODOMA**

**YAH: MAOMBI YA UHAWILISHAJI WA SHAMBA NA. 1172 LILILOPO KIJIJI CHA UCHINDILE WILAYA YA KILOMBERO.**

Tafadhali rejea kichwa cha habari cha hapo juu.

Kijiji cha Uchindile ni miongoni mwa vijiji vilivyokwisha pimwa mipaka ya Vijiji, Kupatiwa Cheti cha Ardhi ya Kijiji na kisha kuandaliwa Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi katika wilaya ya Kilombero. Kijiji hicho kina eneo lenye ukubwa wa **Hekta 53,531.90**, eneo ambalo linatumika kwa shughuli mbalimbali zikiwemo shughuli za uwekezaji.

Mnamo mwaka 2009, Kijiji cha uchindile kilitoa eneo lenye ukubwa wa **Hekta 14,682** kwa kampuni ya **GRL TANZANIA LTD** wakati huo ikiitwa **GREEN RESOURCE LTD,** na kisha eneo hilo kupimwa kwa ajili ya kuanza mchakato wa zoezi la uhawilishaji.

Aidha kampuni tajwa hapo juu, ilipeleka ombi la kupatiwa Ardhi kutoka katika kijiji hiki kwa malengo ya kuendesha shughuli za upandaji miti katika kijiji hicho, ombi ambalo lilifuatiwa na uhitaji wa kufanya uhawilishaji ili Ardhi hiyo iwe chini ya usimamizi wa Sheria ya Ardhi na. 4 ya mwaka 1999 na sio sheria ya Ardhi ya Vijiji na. 5 ya mwaka 1999 kama ilivyo sasa.

Kufuatia uwekezaji wa kampuni hiyo katika kijiji cha uchindile, wakazi wa Kijijini hapo wanategemea kunufaika na mradi huo kupitia kampuni ya GRL TANZANIA LTD ambayo kwa makubaliano ya kisheria imeahidi kufanya yafuatayo kwa wananchi wa kijiji hicho;

WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
IMEPOKELEWA
13 SEP 2018
OFISI YA KAMISHNA MSAIDIZI WA ARDHI - KANDA

a) Ujenzi wa vyoo vyenye jumla ya matundu kumi na sita (16) katika shule ya msingi ya Kihata
b) Ujenzi wa choo cha ofisi ya kijiji
c) Kufunga umeme wa jua katika maabara ya zahanati ya kijiji
d) Ujenzi wa wodi ya Wazazi kwenye zahanati ya Kijiji,
e) Ujenzi wa madarasa mawili katika shule ya msingi ya kihata, pamoja na nyumba moja ya waalimu.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Kilombero, imefanya mawasiliano na kijiji cha Uchindile ili kupata maelezo ya kina kutoka kwa wananchi wa kijiji hicho endapo kuna madai yoyote ya fidia kufuatia kutwaliwa kwa eneo hilo. Hata hivyo uongozi wa kijiji umethibitisha kwamba hakuna madai yoyote ya fidia toka kwa mwananchi yeyote kabla na hata baada ya kuanza kwa mchakato wa kutoa shamba hilo na kwamba shamba hilo lipo maeneo ambayo hayajawahi kumilikiwa na mwananchi yeyote kwa kuwa halifai kwa shughuli za kilimo na kwamba halitumiki kabisa na Kijiji.

**JEDWALI LA TAARIFA MUHIMU ZA KIJIJI CHA UCHINDILE**

| NA. | TAARIFA MUHIMU | TAKWIMU |
|---|---|---|
| 1. | Ukubwa wa kijiji | Hekta **53,531.90** |
| 2. | Idadi ya Wakazi wote Kijijini | 999 |
| 3. | Idadi ya wanaume waliopo kijijini wenye umri wa miaka 18 na Zaidi | |
| 4. | Idadi ya wanawake waliopo kijijini wenye umri wa miaka 18 na Zaidi | |
| 5. | Idadi ya maeneo yaliyokwisha tolewa kwa wawekezaji wengine | GRL TANZANIA LTD<br><br>Hekta 6,647 |
| 6. | Shughuli za uchumi zinazofanyika katika kijiji hicho | -Kilimo<br>-ufugaji<br>- Uvuvi<br>-Biashara |
| 7. | Madhumuni ya uwekezaji huo | Kuendesha shughuli za kilimo |
| 8. | Faida ambazo kijiji kinatarajia kupata kupitia uwekezaji huo | - Ujenzi wa vyoo vyenye jumla ya matundu kumi na sita (16) katika shule ya msingi ya Kihata<br>- Ujenzi wa choo cha ofisi ya kijiji<br>- Kufunga umeme wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | jua katika maabara ya zahanati ya kijiji<br>- Ujenzi wa wodi ya Wazazi kwenye zahanati ya Kijiji,<br>- Ujenzi wa madarasa mawili katika shule ya msingi ya kihata, pamoja na nyumba moja ya waalimu. |
| 9. | Akidi ya Mkutano mkuu wa Kijiji uliopitisha maombi ya Ardhi | Idadi 324 sawa na asilimia 77 |

Kwa barua hii, ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) imeridhika na hatua za awali zilizofuatwa za uhawilishaji wa shamba hilo kuanzia ngazi ya kijiji mpaka wilaya na hivyo kuiomba ofisi yako kuendelea na mchakato wa uhawilishaji wa shamba hilo.

Pamoja na barua hii, naambatanisha nakala za muhutasari wa kikao cha Halmashauri ya Kijiji, Muhtasari wa Mkutano mkuu wa kijiji, Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya kugawa Ardhi ya Wilaya, Taarifa ya Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi ,uthibitisho wa uraia wa wakurugenzi wa kampuni, "Memorandum and Articles of Association", Hati ya usajili, Hati ya uwekezaji, Andiko la mradi, ramani zinazoonesha taarifa mbalimbali za kijiji na za shamba tajwa hapo juu, pamoja na nyaraka zingine muhimu kwa hatua Zaidi za uhawilishaji.

..................................

**SYABUMI GODWIN MWAIPOPO**
**AFISA ARDHI MTEULE**
**Kny: MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**KILOMBERO**

**Nakala:**

GRL TANZANIA LTD
S.L.P 108
**MAFINGA-IRINGA**

MTENDAJI,
KIJIJI CHA UCHINDILE,
S.L.P 580
**IFAKARA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOMBERO**

***(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)***

Simu: 023 - 2931523
Fax: 023 - 2931513
E-mail : ded@kilomberodc.go.tz
E-mail : psded@kilomberodc.go.tz

Idara ya Ardhi na Maliasili
S.L.P. 263,
**IFAKARA.**


**Unapojibu tafadhali taja:-**

Kumb Na. KDC/LD/87128/19/S.G.M 07/09/2018

Kamishna Msaidizi wa Ardhi,
Kanda ya Kati
S.L.P 1062,
**40477 DODOMA**

**YAH: MAOMBI YA UHAWILISHAJIWA SHAMBA NA. 1173 LILILOPO KIJIJI CHA KITETE WILAYA YA KILOMBERO.**

Tafadhali rejea kicha cha habari cha hapo juu.

Kijiji cha Kitete ni miongoni mwa vijiji vilivyokwisha pimwa mipaka ya Vijiji, Kupatiwa Cheti cha Ardhi ya Kijiji na kisha kuandaliwa Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi katika wilaya ya Kilombero. Kijiji hicho kina eneo lenye ukubwa wa **Hekta 25,660.89**, eneo ambalo linatumika kwa shughuli mbalimbali zikiwemo shughuli za uwekezaji.

Mnamo mwaka 2009, Kijiji cha Kitete kilitoa eneo lenye ukubwa wa **Hekta 10,503.03** kwa kampuni ya **GRL TANZANIA LTD** wakati huo ikiitwa **GREEN RESOURCE LTD,** na kisha eneo hili kupimwa kwa ajili ya kuanza mchakato wa zoezi la uhawilishaji.

Aidha kampuni tajwa hapo juu, ilipeleka ombi la kupatiwa Ardhi kutoka katika kijiji hiki kwa malengo ya kuendesha shughuli za upandaji miti katika kijiji hicho, ombi ambalo lilifuatiwa na uhitaji wa kufanya uhawilishaji ili Ardhi hiyo iwe chini ya usimamizi wa Sheria ya Ardhi na. 4 ya mwaka 1999 na sio sheria ya Ardhi ya Vijiji na. 5 ya mwaka 1999 kama ilivyo kwa sasa.

Kufuatia uwekezaji wa kampuni hiyo katika kijiji cha Kitete, wakazi wa Kijijini hapo wanategemea kunufaika na mradi huo kupitia kampuni ya GRL TANZANIA LTD ambayo kwa makubaliano ya kisheria imeahidi kufanya yafuatayo kwa wananchi wa kijiji hicho;


WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
IMEPOKELEWA
13 SEP 2018
OFISI YA KAMISHNA MSAIDIZI WA ARDHI - KANDA

a) Ujenzi wa vyoo vyenye jumla ya matundu nane (8) katika shule ya msingi ya Kitete
b) Ujenzi wa bwalo la chakulala shule ya msingi Kitete
c) Ujenzi wa Kisima cha maji kwa ajili ya Kijiji, kadiri ya utafiti wa wataalamu utakavyoainisha
d) Kufunga umeme wa jua kwenye zahanati ya Kijiji, shule ya msingi kitete na ofisi ya kijiji
e) Ujenzi wa nyumba moja kwa ajili ya kuishi waalimu wawili
f) Ujenzi wa ukumbi wa kijiji
g) Kuchangia vifaa vya michezo kwa ajili ya wanakijiji
h) Kusawazisha uwanja wa michezo wa kijiji
i) Kuchangia pale itakapobidi, vifaa vya kufundishia kwenye shule ya msingi ya kitete. Vifaa hivi ni kama vile vitabu n.k

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Kilombero, imefanya mawasiliano na kijiji cha Kitete ili kupata maelezo ya kina kutoka kwa wananchi wa kijiji hicho endapo kuna madai yoyote ya fidia kufuatia kutwaliwa kwa eneo hilo. Hata hivyo uongozi wa kijiji umethibitisha kwamba hakuna madai yoyote ya fidia toka kwa mwananchi yeyote kabla na hata baada ya kuanza kwa mchakato wa kutoa shamba hilo na kwamba shamba hilo lipo maeneo ambayo hayajawahi kumilikiwa na mwananchi yeyote na kwamba, maeneo hayo hayafai kwa kilimo kwa kuwa ni maeneo ya milimani, na badala yake yanafaa kwa kupandwa miti.

**JEDWALI LA TAARIFA MUHIMU ZA KIJIJI CHA KITETE**

| NA. | TAARIFA MUHIMU | TAKWIMU |
|---|---|---|
| 1. | Ukubwa wa kijiji | Hekta **25,660.89** |
| 2. | Idadi ya Wakazi wote Kijijini | 198 |
| 3. | Idadi ya wanaume waliopo kijijini wenye umri wa miaka 18 na Zaidi | |
| 4. | Idadi ya wanawake waliopo kijijini wenye umri wa miaka 18 na Zaidi | |
| 5. | Idadi ya maeneo yaliyokwisha tolewa kwa wawekezaji wengine | |
| 6. | Shughuli za uchumi zinazofanyika katika kijiji hicho | -Kilimo<br>-ufugaji<br>- Uvuvi<br>-Biashara |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Madhumuni ya uwekezaji huo | Kuendes ia shughuli za kilimo |
| 8. | Faida ambazo kijiji kinatarajia kupata kupitia uwekezaji huo | - Kujenga kisima cha maji cha Kijiji<br>- Kuweka umeme katika zahanati ya kijiji, shule ya msingi kitete na ofisi ya kijiji<br>- Kusaidia kuboresha elimu |
| 9. | Akidi ya Mkutano mkuu wa Kijiji uliopitisha maombi ya Ardhi | Idadl 51 sawa na asilimia 51 |

Kwa barua hii, ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) imeridhika na hatua za awali zilizofuatwa za uhawilishaji wa shamba hilo kuanzia ngazi ya kijiji mpaka wilaya na hivyo kuiomba ofisi yako kuendelea na mchakato wa uhawilishaji wa shamba hilo.

Pamoja na barua hii, naambatanisha nakala za muhutasari wa kikao cha Halmashauri ya Kijiji, Muhtasari wa Mkutano mkuu wa kijiji, Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya kugawa Ardhi ya Wilaya, Taarifa ya Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi ,uthibitisho wa uraia wa wakurugenzi wa kampuni, "Memorandum and Articles of Association", Hati ya usajili, Hati ya uwekezaji, Andiko la mradi, ramani zinazoonesha taarifa mbalimbali za kijiji na za shamba tajwa hapo juu, pamoja na nyaraka zingine muhimu kwa hatua Zaidi za uhawilishaji.

..................................

**SYABUMI GODWIN MWAIPOPO**
**AFISA ARDHI MTEULE**
**Kny: MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**KILOMBERO**

**Nakala:**

GRL TANZANIA LTD
S.L.P 108
**MAFINGA-IRINGA**

MTENDAJI,
KIJIJI CHA KITETE,
S.L.P 580
**IFAKARA**